TANGAZO LA SERIKALI NA. 692 la tarehe 22/9/2023

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA NA 272*)*

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu Na.29 (1) (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MOMBO ("MOMBO WSSA"), KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI ), 2023

Jina

1. Amri hili litajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mombo ("Mombo WSSA"), (Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi ), ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za maji safi za Mombo WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza la Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Kabla ya kutoa ankara kwa kutumia bei na ada zilizoainishwa kwenye Amri hii, Mombo WSSA itapaswa kupeleka ushahidi kwa EWURA kwamba iliwataarifu wateja wake kuhusu agizo jipya la bei na kwamba iliwafahamisha ipasavyo wadau wake ikiwa ni pamoja na viongozi wa serikali, viongozi wa kisiasa, na viongozi wa dini, wateja wake kuhusu mabadiliko ya bei;

(b) Kabla au ifikapo tarehe 31 Oktoba 2023, Mombo WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya

kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hili;

(c) Mombo WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(d) Mombo WSSA itahakikisha kuwa wateja wote wanafungiwa dira za maji ifikapo tarehe 30 Juni 2024;

(e) Mombo WSSA itaandaa na kutekeleza mpango wa kuwafikia wateja wote na kuwasilisha kwa EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(f) Mombo WSSA itahakikisha hesabu zake za fedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi kila mwaka;

(g) Mombo WSSA itashirikiana na Halmashauri ya Mji wa Mombo ili kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka ifikapo tarehe 30 Juni 2025;

(h) Mombo WSSA itahakikisha ina kodi ofisi yenye vyombo vya kutosha kwa wafanyakazi wake wote kabla au ifikapo tarehe 31 Disemba 2023;

(i) Mombo WSSA ihakikishe inaimarisha uongozi wake kwa kuajiri watendaji wake wakuu hususan Meneja wa Ufundi, Meneja wa Fedha na Meneja wa Biashara kabla au ifikapo Juni 2025;

(j) Mombo WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(k) Mombo WSSA kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya

mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Amri hii;

(l) Mombo WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha kama ilivyoidhinishwa katika Jedwali la Nne la amri hii, na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mombo WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake; na

(m) katika kuhakikisha kunakuwepo na huduma endelevu ya maji hususan kipindi cha kiangazi, Mombo WSSA inaelekezwa kuandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua.

Utenguzi T.S Na. la 2011

5. Amri hii inasitisha matumizi ya Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo ("Mombo WSSA"), (Bei za Huduma za Maji safi ), ya Mwaka 2011.

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

*(limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

**BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA**

**Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 395 | 1,000 | 1,100 | 1,100 |
| Taasisi | 390 | 1,000 | 1,100 | 1,200 |
| Biashara | 400 | 1,000 | 1,100 | 1,100 |
| Viwanda | - | 1,290 | 1,400 | 1,400 |
| Magati | 500 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| **WASTANI** | **437** | **1,000** | **1,100** | **1,100** |

**Jedwali Namba 1(b): Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi kwa Mwezi)**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 4,500 | 4,500 | Hairuhusiwi | |
| Biashara | 9,500 | Hairuhusiwi | | |
| Taasisi | 16,500 | | | |
| Viwanda | - | | | |
| Magati | 12,000 | | | |

**Jedwali Namba 1(c): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya gharama za maunganisho mapya kama ilivyoanishwa kwenye kifungu cha 26 cha Kanuni za Usambazaji Maji za Mwaka 2019 | 26,000 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

**Jedwali Namba 1(d): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

**JEDWALI LA PILI**

*(limetengenezwa chini ya aya ya 4 (c))*

**MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA**

| Maelezo | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|
| | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** |
| Kupanua mtandao wa mabomba ya kusambaza maji mjini Mombo kwa kilomita 2 | | 15,000,000 | 15,000,000 |
| Kubadili bomba la urefu wa mita 270 la chuma kuwa la HDPE lenye kipenyo cha milimita 110 na mgandamizo wa mita 160 eneo la Mombo mjini | | | 25,600,000 |
| Kuweka miundombinu ya kutibu maji kwenye chanzo cha Kimweri, matanki la Ndulu na Kikwazu | | 10,000,000 | 10,000,000 |
| Kubadili chemba tatu (3) za valvu eneo la Mbokoi | | 1,650,000 | 1,650,000 |
| Kubadili valvu tano (5) yenye ukubwa wa inchi 4 Mombo mjini | 750,000 | 1,500,000 | 1,500,000 |
| Kubadili mita za maji 224 | 3,120,000 | 13,420,000 | 13,854,700 |
| Kununua na kufunga mita za maji 283 kwa wateja wasio na mita | 36,790,000 | | |
| Kununua na kufunga mita ya maji kubwa ya inchi 6 kwenye chanzo cha maji cha Mbokoi | 800,000 | | |
| Kununua na kufunga mita kwa wateja wapya 1,000 | 5,850,000 | 29,255,600 | 102,109,139 |
| Kununua pikipiki mbili (2) kwa wasoma mita | | 4,000,000 | 4,000,000 |
| Kubadili meza tatu (3) za ofisi | 1,500,000 | | |
| Kubadili vita sita (6) vya ofisis | 1,200,000 | | |
| Kubadili pikipiki mbili(2) | | 8,000,000 | |
| Kununa printa mbili | 200,000 | 200,000 | |
| Kununua kompyuta ya mezani moja | 700,000 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kununua kompyuta mpakato 1 | 3,000,000 | | |
| Kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na kupata hati miliki | | | 12,000,000 |
| **Jumla ya Gharama** | **53,910,000** | **83,025,600** | **185,713,839** |

**J**
**EDWALI LA TATU**

*(limetengenezwa chini ya aya ya 4 (j))*

**VIASHIRIA VYA UTENDAJI**

| **Maelezo** | **Kizio** | **Lengo la Utendaji** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** |
| Idadi ya watu inayofikiwa na huduma ya maji | % | 57 | 80 | 95 |
| Maunganisho mapya ya majisafi | No | 45 | 218 | 737 |
| Upotevu wa Maji | % | 25 | 23 | 20 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 30 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 85 | 90 | 95 |

**JEDWALI LA NNE**

*(limetengenezwa chini ya aya ya 4 (k))*

**MAPATO YANAYOHITAJIKA**

| **Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato (TZS)** | | | |
|---|---|---|---|
| **Maelezo** | **Makisio** | | |
| | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** |
| Uzalishaji | 11,754,007 | 12,621,703 | 13,541,448 |
| Ukarabati na Matengenezo | 73,000,000 | 80,730,000 | 83,555,550 |
| Utawala | 51,368,000 | 78,595,980 | 73,254,764 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Watumishi | 92,800,002 | 119,553,182 | 130,401,897 |
| Matangazo | 8,000,000 | 13,194,000 | 13,394,847 |
| Gharama za Banki | 1,640,040 | 1,702,362 | 1,767,051 |
| **Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo** | **238,562,049** | **306,397,227** | **315,915,558** |
| Uwekezaji wa Miundombinu Mipya | 43,440,000 | 58,255,600 | 143,109,139 |
| Ukarabati na Kubadili Miundombinu | 10,470,000 | 24,770,000 | 42,604,700 |
| **Mapato Yote Yanayohitajika** | **292,472,049** | **389,422,827** | **501,629,397** |
| **Ondoa:** | | | |
| Ada ya Maunganisho Mapya | 1,170,000 | 5,668,000 | 19,162,000 |
| Ada ya Kurejesha Huduma | 2,250,000 | 2,400,000 | 2,550,000 |
| **Mapato Kutokana na Mauzo ya Maji** | **289,052,049** | **381,354,827** | **479,917,397** |

Dodoma, ....................2023,

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*